

Kwa usaidizi wa idhini ya ufahamu



Chanjo inatayarisha kinga za mwili wako dhidi ya virusi na bakteria maalum.

Chanjo itasaidia mfumo wako wa kinga ya mwili kukabiliana vizuri na virusi vinavyosababisha COVID-19.

KWA NINI NIPATE CHANJO?

- > Hulinda dhidi ya COVID-19 na husaidia kuepuka kuwa mgonjwa
- > Hata ikiwa watu wengi wanapona bila kutibiwa, wengine wanaweza kuaga dunia kutokana na COVID-19 au kupata matatizo ya moyo au mapafu kama vile nimonja. Mfumo wa neva pia unaweza kuathiriwa

[Québec.ca/vaccinCOVID](https://quebec.ca/vaccinCOVID)

📞 1 877 644-4545

JE, DALILI ZA MARA KWA MARA BAADA YA CHANJO NI GANI?



Maumivu kwenye sehemu ya sindano



Uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu kwenye misuli au viungo na homa

Hizi ni dalili wastani ambazo hutoweka baada ya siku moja au mbili. Unaweza kumeza dawa ya homa au maumivu kama vile acetaminophen au ibuprofen ili kuziondoa.

JE, KUNA DALILI NYINGINE ADIMU?

Mikabiliano ya mizio ni adimu na ikitokea, kwa kawaida huonekana kwa dakika chache baada ya chanjo wakati wapokeaji bado wanachunguzwa na hivyo itatibiwa mara moja.

Miezi ijayo, mradi tu watu wengi hawatakuwa bado wamechanjwa, COVID-19 itanedelea kuwepo.

Tuendeleo kujikinga!



Kaa mbali na watu wengine



Vaa barakoa



Ziba midomo na pua unapokohoa



Nawa mikono